

KONDOMU YA KIKE YA FC2

NINI Kondomu ya kike ya FC2 ni nini?

FC2 ni kondomu ya kike ambayo ni laini, nyororo na ngumu, iliyotengenezwa kwa nyenzo ya mpira, ambayo huvaliwa ndani ya uke. Ni ya wazi ambayo ina urefu wa sentimita 17 au inchi 6.5 ambayo hukaa FC2 huingia sambamba na uke, ikiruhusu uume kuingia kwa uhuru ndani ya kondomu wakati wa kujamiiana.

INAVALIWAJE

FC2?

FC2 ina pete ya ndani na ya nje. Pete ya ndani inatumika kuingiza FC2 na kuiweka kondomu mahala pake wakati wa kujamiiana. Pete ya nje hubaki nje ya uke. Kama ilivyo kwa kondomu ya kiume, FC2 huzuia shahawa kuingia ndani baada ya kumwaga. Tofauti ni kwamba kondomu ya kike ndiyo njia pekee inayopatikana inayodhibitiwa na wanawake na kuzuia kupata ujauzito usiopangwa na magonjwa ya zinaa, ikiwemo VVU na Zika.

KWANINI

utumie FC2?

FC2 inatoa raha na ulinzi dhidi ya ujauzito na magonjwa ya zinaa katika kifurushi kimoja. Haingiliani na tendo la kujamiiana kwani uingizwaji wake unaweza kufanyika mapema na utoaji wake unaweza kucheleweshwa hata baada ya kujamiiana.

Kwa yeyote yule

- FC2 inatoshea wanawake na wanaume wote bila kujali ukubwa wao au maumbile yao.
- FC2 haina aleji; inawafaa wanaume na wanawake wote ambao wana aleji ya mpira aina ya latex.

Wewe ndio mdhibiti

- Hauhitaji kumuona daktarin kabla ya kuanza kutumia kondomu ya kike.
- Tofauti na njia nyingine za kuzuia mimba, FC2 haidhuru mwili wako. Haina homoni, hivyo haina athari.
- FC2 hutoa kinga ya ziada dhidi ya magonjwa ya zinaa kwa kufunika viungo vya nje vya mwanamke na sehemu ya chini ya uume.

Huongeza raha

- FC2 inatengenezwa kutokana na mpira wa nitrile, ikimaanisha kwamba – tofauti na kondomu zinazotengenezwa kwa mpira wa latex – inaweza kutumika kwa mchanganyiko na mafuta-, maji-, au vilainishi jamii ya silicone bila kuathiri usalama wake
- FC2 inabadilika kutokana na joto la mwili, ikifanya kujamiiana kuwa na joto na asili
- FC2 imewekewa vilainishi vya hali ya juu vya silicone.
- Kwa baadhi ya watumiaji, pete zile mbili zinaweza kuongeza raha zaidi, muamko wakati wa kujamiiana

WAKATI

gani wa kuingiza FC2?

- FC2 inaweza kuingizwa aidha masaa machache au mara tu kabla ya kujamiiana
- Uume huitaji kuwa umesimama ili utumie FC2, na sio lazima uondolewe mara tu baada ya kujamiiana.

NANI


anaweza kutumia FC2?

FC2 inaweza kutumiwa na wanawake na wanaume wote ambao wanataka kushiriki tendo la kujamiiana. FC2 inaweza kutumiwa na:

- Wanawake walio katika hedhi, Wajawazito, ambao wanakaribia au wamepita menopause
- Wanawake ambao wamejifungua karibuni, na ambao wamefanyiwa upasuaji kutoa uterasi
- FC2 inaweza kutumiwa pamoja na kidonge, sindano, lupu, kitanzi, na Vasektomi kutoa ulinzi dhidi ya magonjwa ya zinaa, ikiwemo VVU na Zika.



JINSI YA KUTUMIA FC2?




Sambaza kilainishi





Fungua kifurushi



Shika na bonyeza pete ya ndani



Ingiza kondomu ya kike



Ingiza kondomu ya kike



Ungependa kujifunza zaidi?

www.fc2femalecondom.com | info@fc2femalecondom.com |

f @FemaleCondomFC2

| t @FC2FemaleCondom

| y FC2FemaleCondom